# RIPOTI YA YA KUKABILIANA NA PENGO LA JUHUDI ZA KUKABILIANA NA UZALISHAJI WA GESI CHAFU YA MWAKA WA 2023, UJUMBE MUHIMU UNAOWASILISHWA

ISICHAPISHWE KAMWE
Isichapishwe wala kusambazwa kabla ya
6:00am EST/1:00pm EAT/11:00am CET, Novemba 2, 2023

***Ripoti ya UNEP ya Kukabiliana Na Pengo la Juhudi za Kukabiliana na Uzalishaji wa Gesi Chafu ya Mwaka wa 2023: Hakuna ufadhili wa kutosha,* wala maandalizi ya kutosha *– Uwekezaji duni na mikakati duni ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni hatari kwa dunia* inaonyesha kuwa hatua za kukabiliana na hali zinapungua katika nyanja zote badala la kuongezeka ili kuweza kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi zinazozidi kuongezeka.**

- Katika mwaka wa 2023, joto liliongezeka na kuvunja rekodi, huku dhoruba, mafuriko, kiangazi na mawimbi ya joto vikisababisha uharibifu. Athari hizi zinazoongezeka zinaonyesha umuhimu wa kuimarisha juhudi za kulinda walio hatarini kwa dharura, mbali na kupunguza uzalishaji wa gesi ya ukaa kwa dharura.
- Hata hivyo, hatua za kukabiliana na hali zinapungua katika maeneo yote matatu yaliotathminiwa: ufadhili, mikakati na utekelezaji.
- Hatua za polepole na zisizotosha za kupunguza na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi zinaendelea kuchangia kwa kasi kwa mapungufu ya kukabiliana na hali, licha ya baadhi ya hatua zilizokuwa zimepigwa.
- Kushindwa huku kukabiliana na hali kikamilifu kunazidisha janga la mabadiliko ya tabianchi na kuna athari kubwa kwa hasara na uharibifu, haswa kwa walio hatarini zaidi.

**Masasisho ya gharama za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika nchi zinazoendelea inakadiriwa kuwa dola za Marekani kati ya bilioni 215 na bilioni 387 kwa mwaka katika muongo huu.**

- Ripoti hii imefanyiwa marekebisho makubwa na sasa inakadiria gharama kubwa zaidi za ukabilianaji wa hali kuliko tafiti za awali.
- Gharama za miradi ya kukabiliana na hali hii katika nchi zinazoendelea zinakadiriwa kuwa dola za Marekani bilioni 215 kwa mwaka katika muongo huu na zinatarajiwa kupanda kwa kasi kufikia mwaka wa 2050.
- Fedha za kukabiliana na hali zinazohitajika ili kutekeleza vipaumbele vya kukabiliana na hali hii ndani ya nchi, kwa kuzingatia kuongezeka kwa Michango Inayoamuliwa na Taifa na Mipango ya Kitaifa ya Kukabiliana na hali katika nchi zote zinazoendelea, inakadiriwa kuwa dola za Marekani bilioni 387 kwa mwaka kati ya 2021 na 2023.

**Mahitaji ya kifedha ya kukabiliana na hali katika nchi zinazoendelea ni kati ya mara 10 na 18 zaidi kwa kuzingatia mtiririko wa kimataifa wa fedha za umma – asilimia 50 zaidi kuliko makadirio ya hapo awali.**

- Mtiririko wa fedha za kukabiliana na hali za mashirika ya kimataifa na baina ya nchi mbili kwa nchi zinazoendelea ulipungua kwa asilimia 15 hadi takribani dola bilioni 21 katika mwaka wa 2021.

- Hali hii inajiri licha ya ahadi zilizotolewa katika COP26 mjini Glasgow za kuongeza maradufu ufadhili wa kukabiliana na hali wa mwaka wa 2019 hadi karibu dola bilioni 40 kwa mwaka kufikia mwaka wa 2025, hali inayotisha.
- Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya kifedha ya kukabiliana na hali kupungua kwa pesa zinazotolewa, hali ya sasa ya pengo la ufadhili linakadiriwa kuwa dola za Marekani bilioni kati 194 na 366 kwa mwaka.

**Mikakati na utekelezaji wa juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi inaonekana kuwa mibovu licha ya juhudi za kukabiliana na hali zilizoongezeka.**

- Ingawa nchi tano kati ya sita zina angalau chombo kimoja cha kitaifa cha mikakati ya kukabiliana na hali, hatua za kufikia utekelezaji wa kimataifa kikamilifu zinapungua, na zinahitaji kuimarishwa zaidi.
- Zaidi ya nusu ya Nchi Wanachama wa Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi zina vyombo viwili au zaidi vya kisheria vya ngazi ya kitaifa. Hatua kwa kiasi kikubwa kwa hivyo inapaswa kuzingatia utoshelevu na ufanisi.
- Idadi ya hatua za kukabiliana mabadiliko ya tabianchi kwa msaada wa mifuko nne ya fedha ya kimataifa ya kufadhili mabadiliko ya tabianchi ni ndogo kuliko mwaka jana, pengine kutokana na COVID-19 na vita nchini Ukraine. Kiwango cha hatua za kukabiliana na hali zilidumaa katika muongo uliopita.

**Kutokana na kupungua kwa upunguzaji na ukabilianaji wa hali, hasara na uharibifu unaotokana na mabadiliko ya tabinchi unaongezeka.**

- Ripoti ya hivi karibuni inaonyesha kuwa chumi 55 zilizo hatarini zaidi kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi tu tayari zimepata hasara na uharibifu wa zaidi ya dola za Marekani bilioni 500 katika miongo miwili iliyopita.
- Gharama hizi zitapanda kwa kasi katika miongo ijayo, hasa kwa kukosekana kwa mikakati kapambe ya kupunguza na kukabiliana na hali, ila idadi kubwa zaidi inahitajika ili kushughulikia hasara na uharibifu kwa dharura.
- Mfuko mpya wa kukabiliana na Hasara na Uharibifu utakuwa chombo muhimu cha kukusanya rasilimali, ila changamoto zitasalia. Mfuko utahitaji kuzingatia mbinu bunifu zaidi za ufadhili ili kufikia kiwango kinachohitajika cha uwekezaji.

**Kuwekeza kwa kupunguza na kukabiliana na hali kutapunguza gharama za kushughulikia mazingira katika siku zijazo.**

- Ukabilianaji wa hali kwa njia madhubuti unaweza kuimarisha ustahimilivu - ambayo ni muhimu hasa kwa nchi za mapato ya chini na makundi yaliyo hatarini - ikijumuisha wanawake.
- Utafiti unaonyesha kuwa kila bilioni iliyowekezwa katika kukabiliana na mafuriko katika maeneo ya pwani husababisha kupungua kwa gharama za liuchumi za kushughulikia uharibifu kwa dola za Marekani bilioni 14.
- Wakati uo huo, dola bilioni 16 kwa mwaka zikiwekezwa katika kilimo zinaweza kuzuia takriban watu milioni 78 dhidi ya njaa au baa la njaa kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**Kutafuta njia bunifu za kutoa ufadhili wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni muhimu - kwa kuzingatia ukabilianaji wa hali unaotarajiwa na ufanisi wake.**

- Lengo la mwaka wa 2019 la kuongeza maradufu ufadhili wa kimataifa kwa nchi zinazoendelea kufikia mwaka wa 2025 wala Lengo Jipya la Takwimu za Pamoja kufikia mwaka wa 2030 havitaweza kuziba pengo la kifedha la kukabiliana na hali kwa kiwango kikubwa kivyake.
- Ripoti hii inabainisha njia saba za kuimarisha ufadhili, ikiwemo kupitia matumizi ya ndani ya nchi na ufadhili wa kimataifa na wa sekta binafsi.
- Njia za ziada ni pamoja na utumaji fedha kama zawadi, kuongeza na kutoa ufadhili kwa Mashirika ya Biashara Madogo na ya Kati, utekelezaji wa Kifungu cha 2.1(c) cha Mkataba wa Paris kuhusu kubadilisha mtiririko wa fedha kuelekea njia za maendeleo zinazozalisha hewa ya ukaa kidogo na kustahimili mabadiliko ya tabianchi, na kufanyia mabadiliko mfumo wa ufadhili duniani, kama ilivyopendekezwa na Mpango wa Bridgetown.

**COP28 ni sharti iimarishe juhudi za kukabiliana na hali na hasara na uharibifu.**

- Mfuko wa Hasara na Uharibifu na majadiliano yanayoendelea ya kuanzisha Lengo Jipya la Takwimu za Pamoja kuhusu Ufadhili wa Mazingira ni juhudi muhimu za kufaulisha.
- Pamoja na Tathmini ya Kwanza ya Kimataifa, kupiga hatua kuu za kufikia malengo haya katika COP28 kunaweza kufahamisha Lengo la Kimataifa la Kukabiliana na hali na kutoa mfumo thabiti zaidi wa mahitaji ya fedha za kukabiliana na hali, bila kupoteza mwelekeo wa na kuimarisha ukabilianaji wa hali.
- Watunga sera, benki za kimataifa, wawekezaji na sekta ya kibinafsi watumie fursa ya COP28 kama wakati ambapo ulimwengu utajitolea kikamilifu kuhami nchi za kipato cha chini na makundi yaliyo hatarini, kama vile wanawake na Watu wa Kiasili, dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi.